



AHMAD AL-RAYSUNI

AL-SHUURA

*Kanuni ya Qur'an ya Kufanya
Uamuzi kwa Kushauriana*

■ SWAHILI VERSION

Idara ya Lugha na Ukalimani ya Chuo Kikuu
cha Waislamu cha Morogoro

IIIT — Mfululizo wa Vitabu kwa Muhtasari

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa
Rehema, Mwenye Kurehemu

KUHUSU MWANDISHI

AHMAD AL-RAYSUNI ana digrii ya Uzamivu katika Taaluma za Dini ya Kiislamu kutoka katika Chuo Kikuu cha Muhammad al-Khamis, Rabat, nchini Morocco. Amefanya kazi katika Wizara ya Sheria, ni mhariri wa gazeti la al-Tajdid, na ni mwanachama Jumuiya ya Wanazuoni wa Kiislamu nchini Morocco.

Profesa al-Raysuni ameandika vitabu vingi na makala nyingi katika *al-Maqaid* kwa Kiarabu, ambazo miongozi mwazo zimetafasiriwa katika lugha nyingine. Kwa sasa Profesa Raysuni anafundisha Usul al-Fiqh na Maqasid al-Shari'ah katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii katika Chuo Kikuu cha Muhammad al-Khamis, Morocco.

AHMAD AL-RAYSUNI

AL-SHUURA

Kanuni ya Qur'an ya Kufanya

Uamuzi kwa Kushauriana

■ SWAHILI VERSION

Idara ya Lugha na Ukalimani ya Chuo Kikuu
cha Waislamu cha Morogoro

©International Institute of Islamic Thought, 2012

International Institute of Islamic Thought (IIIT)

P.O.Box 669

Herndon, VA 20172, USA

www.iiit.org

16 / 03/ 1429 AH 24/ 03/ 2008 AD

Hakimiliki ya Kitabu hiki imehifadhiwa. Hairuhusiwi kukipiga chapa, kwa namna yoyote ile bila ruhusa ya maandishi ya wachapaji.

Rai na maoni yaliyo elezwa katika kitabu hii ni ya mwandishi, na siyo kwamba ndio mtazamo wa wachapaji.

Kimetafsiriwa na:

Sadiki Moshi Feruzi

Kimehaririwa na:

Fatuma R. Kawale

Maryam Y. Mwinyi

Design and layout by:

Iddi Suleiman Kikong'ona (iddkiko@gmail.com)

Neno la Awali

MFULULIZO WA MUHTASARI WA VITABU VYA IIIT

Mfululizo wa muhtasari wa vitabu vya IIIT¹ ni hazina muhimu sana katika machapisho ya taasisi hii vilivyoandikwa kwa ufupi kabisa ili kumwezesha msomaji kuelewa dhamira kuu ya kitabu asilia. Vitabu vimeandikwa kwa ufupi ili kusomeka kwa urahisi na kuokoa muda hasa kwa waliotingwa na kazi. Machapisho haya yanatoa mwongozo wa dhima kuu, hivyo kumfanya msomaji kuwa na ari ya kutafuta nakala ya kitabu chenyewe.

Kitabu halisi cha “Shuura: Kanuni ya Qur’an ya kufanya Uamuzi kwa Kushauriana” alichandika Ahmad al-Raysun, kilichapishwa mwaka 2011. Waislamu, kwa kiwango kikubwa hawakutambuwa umuhimu na thamani ya kanuni ya Shuura iliyomo kwenye Qur’an, pamoja na kazi kubwa inayoweza kufanya katika kuiendeleza na kuijenga upya jamii ya Kiislamu.

Katika kitabu hiki, mwandishi amethubutu kubainisha maana halisi ya Shuura na kuchambua vipengele vya utekelezaji wake. Amedhirisha chimbuko la Shuura na kuonesha namna ambavyo kanuni hii inavyoweza kuingizwa, kutekelezwa katika taasisi na jumuiya, na kutumiwa na jamii za Waislamu kwa ujumla.

1. Ni ufupisho wa *International Institute of Islamic Thought* iliyo tafsiriwa kwa Kiswahili kama Taasisi ya Kimataifa ya Fikra ya Kiislamu

Hapana shaka kabisa kuwa, kwasababu anuai za kihistoria na kisiasa, ulimwengu mzima wa Kiislamu umeiweka Shuura kando, hawaitumii.

Kwa mujibu wa mwandishi, japokuwa mambo mengi juu ya mada hii yameandikwa, kiuhalisia hakuna lililotekelezwa zaidi ya kupuuzwa. Hata zama hizi, utambuzi wa dhana na kazi ya Shuura ni suala linalo jadiliwa kwa ushindani mkubwa wa hoja. Mtazamo wa kuinasibisha Shuura na ushirikishaji wa kidemokrasia katika mchakato wa maamuzi umekuwa ukistawi zaidi na kuibuwa malumbano yanayo kosoa mtindo huo wa kuilinganisha Shuura na fikra za kimagharibi kuhusu dekmokrasia. Wapo pia wenye mtazamo kuwa kanuni hizi ni namna tu ya kueleza dhana ya kugatua madaraka.

Mambo haya na mengine mengi yamefanyiwa utafiti makini wa kitaalamu. Mwandishi Al-Raysuni anahitimisha kwa kusema kwamba, Waislamu lazima waifanye Shuura kuwa sehemu muhimu ya mfumo wao wa maisha ili kulinda maslahi yao, na kwamba Shuura ni zana muhimu kwa wao kuweza kujijenga na kujiimarisha upya. Kwa namna hii, mwandishi analichambua suala hili kwa mtazamo mpya, wenye kutoa mwangaza katika vipengele ambavyo hadi sasa ni vichache vilivyotizamwa, ikiwa vilichunguzwa.

Toleo lililofupishwa kutoka katika toleo asilia

AL-SHUURA: Kanuni ya Qur'an ya Kufanya
Uamuzi kwa Kushauriana

Ahmad al-Raysuni

ISBN hbk: 978-1-56564-362-8

ISBN pbk: 978-1-56564-361-1

2012

Yaliyomo



NENO LA AWALI

Mfululizo Wa Muhtasari Wa Vitabu Vya IIIT...v

UTANGULIZI

viii

SURA YA KWANZA

Mazingira ya Shuura Katika Maisha 1

SURA YA PILI

Mambo ya Kuzingatia wakati wa Shuura 8

SURA YA TATU

Chimbuko la Shuura na Historia yake 14

SURA YA NNE

Tunawezaje kuhamasisha kuitekeleza Shuura? 18

HITIMISHO

24

MAELEZO YA PEMBENI

25

Utangulizi



Shuura, kama ilivyotajwa ndani ya Qur'an na kudhihiri katika utendaji wa Mtume Muhammad (s.a.w) na Maswahaba zake, ni chombo muhimu kwa ujenzi mpya, mageuzi na uimarishaji wa jamii kupitia Uamuzi wa pamoja uliofikiwa kwa njia ya ushauri na majadiliano. Lakini Waislamu, kwa kiwango kikubwa hawajui umuhimu na thamani ya Shuura hali ambayo hata ulamaa au wasomi wa kiislamu hawana hakika ya wakati gani inakuwa lazima kutumika kanuni hii na kwa masuala yepi yatahitajia kufanya Shuura.

Katika mazingira na muktadha wa zama hizi, Shuura imekuwa ikinasibishwa na ushiriki wa kidemokrasia katika mchakato wa kuweka maamuzi, ikihusishwa hususan, na mwongozo wa Qur'an na Sunnah. Aidha, upande mwingine unatowa changamoto kwa kukosoa mtazamo wa wanaolinganisha *Shuura* na demokrasia. Hata hivyo, ulimwengu wa Kiislamu, kwa ujumla, umezama kwenye tope zito la siasa za kibabe na utawala wa kiimla, hivyo hapana budi kufuata Shuura katika mfumo wa maisha ili kulinda maslahi binafsi na ya jamii; na kuifanya kuwa nyenzo ya ujenzi mpya na uboreshaji.

Kitabu hiki kimeitafiti kanuni hii ya Shuura na kubainisha namna inavyoweza kuingizwa kwenye utendaji na kutumiwa katika jamii za Waislamu na maisha yao.

Dhana ya Shuura kama nyenzo ya kuwezesha kufikia Uamuzi wa pamoja kwa njia ya ushauri na majadiliano imekuwa bado haijaleleweka vyema licha ya kuwepo jitihada kubwa katika zama hizi za kuchapa maelfu ya vitabu na makala kujadili dhana hiyo. Ni dhahiri kwa muktadha huu kuwa yapo mambo mengi kuhusu Shuura bado yanahitaji kuelezwa. Kitabu hiki kimelenga kufafanua msingi wa dhana ya Shuura na kuonesha namna utekelezwaji wake unavyoweza kuinua jitihada na kuzielekeza katika kuinufaisha jamii ya Kiislamu duniani.

Chemchem za msingi wa manhaji na kanuni za kitabu hiki ni aya za Qur'an tukufu na matukio katika maisha ya Mtume (s.a.w) na utendaji wa kugezwa katika maisha ya maswahaba waongofu. Matini ya aya anuai kutoka katika Qur'an na Hadithi zinazo bainisha Sunna ya Mtume (s.a.w) zinaidhihirisha Shuura kuwa ni nyenzo muhimu katika nyanja zote za maisha ya watu; kiroho na kimwili, iwe mtu mmoja mmoja au kikundi.

Sura ya Kwanza



MAZINGIRA YA SHUURA KATIKA MAISHA YA KIISLAMU

Linapojadiliwa suala la Shuura na ushahidi unaothibitisha uhalali wake katika vitabu vya sheria za Kiislamu, wasomi na waandishi husimamia aya mbili za Qur'an. Aya ya 38 iliyomo kwenye surat Shuura (42) na aya ya 159 katika Surat Al-Imraan (3). Aya hizi zinaelezea mazungumzo ya Allah (s.w)² na malaika juu ya kuumbwa kwa Adam na hatma ya kizazi chake hapa duniani.

Msomi mashuhuri Muhammad al-Tahir ibn Ashur anasema kuwa Mwenyezi Mungu alifanya mjadala huu ili kuwapa heshima na kuwaelimisha malaika, pia kuwatia ari ya ushindani. Aidha, Shuura ilitazamiwa kufanywa mwanzo kabisa wa uumbaji ili iwe mwongozo kwa binadamu.

Tukio jengine linalohusishwa katika sehemu hii ni kushauriana kwa nabii Ibrahim na mwanawe (Ismail) kuhusu amri aliyopewa na Mwenyezi Mungu. Suala la nabii Ibrahim kumtoa muhanga mwanawe tayari limeelezwa vizuri katika Qur'an. Hata hivyo, nabii Ibrahim alimuuliza mwanawe,

فَانظُرْ مَاذَا تَرَىٰ ۗ قَالَ يَأْتِيَنَّكَ مِنْهُمُ
بَشَرٌ مِّنْ النَّاسِ ۗ قُلْ إِنِّي لَأَخْلَقُ لَهُم مِّمَّا يَخْلُقُ الْإِنسَانَ ۚ إِنَّ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ

2.(s.w) – Subhanahu wa Ta'ala: Ametakasika na Ametukuka. Husemwa anapotajwa Mungu.

“unaonaje juu ya jambo hili?” Mwanawe alimjibu; “Baba! Tafadhali fanya kama ulivyoamrisha, Mwenyezi Mungu akipenda utanikuta miongoni mwa wale wenye kusubiri”

(Sura Al-Saffat 37:102).

Ingawa nabii Ibrahim alipewa amri nzito na Mwenyezi Mungu ya kumtoa muhanga mwanawe, bado alifanya Shuura na mwanawe juu ya jambo hilo.

Vitabu vyengine vingi vimetoa ushahidi wa aya anuai za Qur'an zinazoeleza misingi ya kuwa na Shuura katika maisha ya kila mtu: baina ya mume na mke, baina ya wazazi na watoto, na hata kwa mambo yanayohusu ndoa na talaka. Malengo mengi tunayojiwekea na faida kubwa tunaweza kuipata endapo tutafanya Shuura. Ikiwa tutafuata mtazamo alioueleza Ibn Ashur na wanazuoni wengine aliowanukuu, Shuura ndiyo nguzo ya matendo ya kijamii ambayo Allah (s.w) alimjengea mwanadamu. Katika mfano mwingine, “majadiliano na kupata uamuzi wa pamoja” ni suala lililotajwa katika aya za Qur'an, kuhusu majadiliano baina ya wazazi kukubaliana juu ya kumkatisha mtoto au kuendelea kumnyonyesha, kwa mfano:

فَإِنْ أَرَادَا فِصَالًا عَنِ تَرَاضٍ مِّنْهُمَا وَتَشَاوُرٍ
فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا

“...Na wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa kwa kuridhiana na kushauriana, basi si vibaya kwao...”

(Qur'an 2:233).

Hivyo basi, masuala ya malezi ya mtoto yanayozingatia makubaliano ya pamoja ni haki na wajibu kwa wazazi wote wawili, ili kuhifadhi ustawi wa mtoto. Makubaliano haya yanayozingatia kwa umakini sana masuala ya mtoto, yanasaidia kumlinda mtoto na hivyo ni ishara ya huruma na rehema za

Mwenyezi Mungu. Malezi yanahitaji Shuura baina ya wazazi au baina ya wazazi na watoto wao ikiwa wamefikia utu-uzima. Pia inashauriwa wazazi kuweka utaratibu wa kuwashirikisha watoto wao katika maamuzi ili kuwaonesha kuwa Shuura ndiyo msingi wa maisha. Pia, Shuura hufanywa katika mambo yanayohusiana na ndoa, mambo ya kifamilia kama malezi ya watoto na mazingira yanayotawaliwa na migogoro.

Shuura ni katika mifano ya mambo yanayostahiki kuigwa hata kama ni katika mambo ambayo tayari yanahitaji uamuzi au majibu yake yanafahamika. Shuura ina malengo na faida mahususi, miongoni mwazo ni kupata maridhiano ya pamoja, kutoa maelekezo, kuhifadhi heshima pia ni kielelezo kizuri cha kuigwa na wengine. Ikiwa Shuura ni jambo linalosisitizwa hata juu ya mambo ambayo tayari yameshatolewa ufumbuzi, basi ni jambo muhimu sana na la lazima katika mambo changamani au mazito yanayotatiza mitazamo ya watu.

Shuura ni muhimu pia katika mambo binafsi, ikiwemo mambo ya mtu binafsi, mtu binafsi na uhusiano wake na watu wengine, baina ya mume na mke na wazazi na watoto wao. Ni muhimu vilevile kwa mambo ya kijamii na mambo kadhaa yatokanayo na kuamiliana kwao. Umuhimu wa Shuura kijamii umeelezwa wazi katika aya mbili za Qur'an zilizotangulia. Aya zinawazungumzia wale

وَأْمُرْهُمْ شُورَىٰ بَيْنَهُمْ

"ambao uongozi [katika mambo yote muhimu na ya pamoja] ni kwa kushauriana baina yao"

(Al-Al-Shuura, 42:38)

فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ

*Basi wasamehe, na waombe maghfira, na shauriana
nao katika mambo. (Al-Imran 3:159).*

Shuura imeelezwa kwa upana zaidi katika Sura ya 42 pamoja na sifa za msingi za waumini ambao hushauriana baina yao katika mambo yote muhimu. Wanazuoni wanaeleza kuwa pamoja na sifa nyingine nyingi, Shuura ni kigezo muhimu na ndio msingi wa dini ya Kiislamu.

Katika sura ya 3:159 Mtume wa Mwenyezi Mungu anaambiwa kwa kadiri ya uwezo wake kuwa muongozaji, muelimishaji, amiri jeshi, kiongozi na mlinganiaji katika kumuamini Mwenyezi Mungu. Kazi hii ilimtaka awe mpole, mnyenyekevu na mvumilivu kwa watu wengine, kuvumilia hisia za watu wengine na mwenye kusamehe anapokosewa, hivyo hivyo, mambo hayo yanamtaka ashirikiane na watu wengine na kuthamini maoni yao. Pamoja na kuwa amri hii ya kufanya Shuura amepewa Mtume wa Mungu na maswahaba wake, pia inawahusu wale wote wanaompenda Mtume, amiri jeshi, viongozi na walinganiaji. Aya hii inatazamwa kama kanuni muhimu katika serikali na utawala wa Kiislamu na katika uhusiano baina ya viongozi Waislamu na wale wanaowatawala.

Swahaba wa Mtume Abu Hurayrah anasema “Sikuwahi kuona mtu yeyote aliyekuwa akiwataka maswahaba kukaa Shuura kama Mtume Muhammad (s.a.w)³”. Katika sheria za Kiislamu ni amri kukaa Shuura kwa mambo yote ya kijamii. Pia, magavana, marais na wale wote wenye mamlaka kwao Shuura ni wajibu. Ilimuwajibikia Mtume Muhammad (s.a.w), hivyo ni lazima kwa wafuasi wake pia.

Maneno ya Mwenyezi Mungu kwamba “wale ambao hukaa Shuura katika mambo yao” yanatuonyesha kuwa mambo yote

3. Imesimuliwa na al-Tirmidhī katika moja ya milango yake ya jihadi.

yanayoihusu jamii kwa jumla lazima yaamuliwe katika Shuura. Kwa namna hiyo, hakuna hata mmoja akiwemo imamu na viongozi wengine, mwenye haki ya kulifanya jambo linaloihusu jamii nzima kama lake peke yake. Ulazima wa Shuura unatokana na faida au madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na maamuzi.

Kwa kuzingatia mifano kutoka kwa Mtume (s.a.w) kama ilivyoelezwa na wanazuoni, Shuura inapaswa kutumika katika siasa na maeneo mengine yote. Kanuni hizo hizo zitumike kwa kila mtu na katika kila nafasi anayoitumikia iwe ni hakimu au kiongozi. Nyanja muhimu sana ambapo Shuura haina budi kutumika ni katika siasa, utumishi na jeshi. Hata hivyo, kuna wakati Shuura si lazima kuzingatiwa ikiwa sheria za dini zimeelezwa vizuri, kwa uwazi na upana wake.

Aidha, eneo ambalo Shuura ni lazima (kutumika) ni pale endapo jambo linalotatiza halina maelezo ya kutosha katika Qur'an na hivyo hutatuliwa kwa kuzingatia qiyas, mawazo ya wanazuoni (istihsan), na kwa kuzingatia maslahi ya umma (istislah). Ibn Abd al-Barr anasimulia kuwa Ali ibn Abi Talib alisema "nilisema, Eeh Mtume wa Allah, tutafanyaje ikiwa kuna jambo ambalo halijaelezwwa katika Qur'an na hatukupata kuona kutoka kwako?" Mtume akamjibu "kaeni Shuura baina yenu waumini mlio na elimu. Hivyo Shuura baina yenu ni jambo la muhimu sana na kamwe msiegeme mawazo ya mtu mmoja".⁴ Ibn Umar anasema kuwa Shuura ilitumika kuboresha utamaduni wa adhana, au wito wa sala⁵. Mtume alishauriana na Maswahaba wake namna bora ya kuwaita waumini katika sala. Katika hili hakusubiri wala kuomba mwongozo au maelezo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, haikuwa kawaida ya Mtume Muhammad (s.a.w) kuwataka ushauri Maswahaba wake

4. Imesimuliwa na al-Tirmidhī katika moja ya milango yake ya jihadi.

5. Ingawa kulikuwa na udhaifu katika mlolongo wa masimulizi haya maudhui yake yamethibitishwa kuwa ya kweli na yakuaminika, pia, 'Abu 'Umar ibn 'Abd al-Barr, Jamii' Bayan al-Ilm wa Fadlihi wa Yanbaghi fi Riwayatihi wa Hamlihi (Beirut: Dar al - Fikr, hakuna tarehe), 2/73.

katika mambo ya msingi yanayohusu sharia. Alikuwa akipokea maneno matukufu ambayo yalikuwa ndio chanzo kikuu katika mambo kama hayo. Hata hivyo bado alikuwa akiwataka ushauri watu wengine katika masuala kama haya ili iwe mfano wa kufuatwa kwa vizazi vijavyo.

Vilevile, Shuura ni nyenzo muhimu katika masuala ya hukumu katika maisha ya Muislamu – uongozi wa hakimu unaathiri wote, iwe mtu mmoja mmoja na makundi, na pengine hata mataifa na serikali. Hadithi na matendo ya Mtume yanayohusiana na Shuura hutumika pia katika maeneo yasiyokuwa na ufafanuzi katika Qur'an na Sunna, na kwamba katika hali kama hii Makhalifa na Maswahaba walitumia Shuura kutatua migogoro. Hakika kanuni hii pia ndiyo inayotumika kwa kila mtu katika nafasi ya uongozi au uhakimu.

Wakati mashitaka yalipomfikia Abu Bakar al-Siddiq, kwanza aliweza kutazama katika Qur'an. Ikiwa Qur'an imetowa hukumu juu ya jambo hilo basi hiyo ndiyo hukumu aliyotekeleza. Ikiwa Qur'an haikuzungumza lolote basi alirejea maelekezo ya Mtume na kutoa hukumu kwa kuzingatia maelekezo hayo.⁶ Vinginevyo aliwauliza watu ili kupata ufumbuzi. Ikiwa suluhisho halikupatikana alikuwa akiwaita wanazuoni wa Kiislamu na viongozi katika Shuura na kisha alitumia makubaliano ya Shuura kutoa hukumu.

Aidha, katika kuongezea matumizi ya Shuura na kusisitiza umuhimu wake, Uislamu unasisitiza na kupendekeza Waislamu kuitumia (Shuura) kivitendo. Na kwa wakati huo huo Uislamu unaupa mamlaka Umma wa Kiislamu kuitumia, kuifanya katika usahihi wake, kuchukua kanuni kwa matumizi katika nyakati tofauti tofauti, maeneo mbalimbali, tawala mbalimbali na mazingira mbalimbali katika ushauri ulio huru na usimamizi mzuri. Pia, utekelezaji wa kina unamaanisha kutumia kanuni za Shuura katika maisha ya Waislamu ni kwao wenyewe kuwa

6. Sahih al Bukhari, Kitabu cha wito wa Sala (kitab al-adhan), na al-Tirmidhi, Mlango wa Sala (abwab al-Sala).

tayari kutumia Shuura na pia kutumika katika taasisi zote na shughuli zote za kiutawala, kijamii na jumuiya ndogo ndogo za Waislamu.

Kazi na sababu mbalimbali zinafanikishwa kupitia Shuura iliyoanzishwa na Uislamu. Mwanasheria wa Hanafi, Abu Bakar al-Jassas anataja faida za Shuura katika Uislamu kuwa ni pamoja na: hutoa hukumu iliyowazi juu ya jambo ambalo halijaelezwa katika Qur'an; hutoa taashira juu ya msimamo wa maswahaba wa Mtume ambao mitazamo yao ni ya kuigwa; pia inashajiisha matumizi ya akili katika kufikia maamuzi (sahihi)⁷.

Mwanasheria wa Maliki, Abu Bakr ibn al-Arabi alieleza kuwa faida ya Shuura inatoa fursa ya kuchukua hatua kulingana na kitu kinachojulikana; kwamba, ukweli umeachwa huru kutoka katika matamania mabaya ya watu; na kwamba maamuzi yanatokana na mawazo ya watu na uwezo wao wa kufikiri.⁸ Kwa ujumla Shuura ina faida zifuatazo:

- Hubainisha matendo mazuri
- Huondosha uonevu na ubinafsi
- Huzuia udhalimu
- Hufundisha unyenyekevu
- Hutoa haki kwa kila mmoja
- Huhimiza mazingira ya uhuru na ubunifu
- Hukuza uwezo wa kufikiri na kupanga mipango
- Huchochea utayari wa kutekeleza jambo
- Huhimiza umoja
- Utayari wa kupokea machungu ili kupata maslahi ya umma

7. Muhammad Ruwwas Qalaji, Mawsu 'at Fiqhi Abi Bakar al-Siddiq (Beirut: Dar al Nafa'is, 1994), uk. 155.

8. Abu Bakar al Jassas, Ahkam al Qur'an, 2/41.

Sura ya Pili



MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA KATIKA KUFANYA SHUURA

Sheria za Kiislamu hazijaweka masharti na vigezo juu ya utekelezaji wa Shuura. Zimetoa fursa kwa watu kutumia busara, uchaguzi wao wenyewe na makubaliano. Shuura inaonekana kuwa na maeneo mengi ya kutumika hivyo labda ikiwa kuna jambo ambalo ni mahususi, litahitaji watu wenye ujuzi na uzoefu juu ya jambo hilo.

Shuura juu ya mambo ya umma inahusisha kuweka mipango, kuendeleza masuala ya taifa, jamii na jumuiya na makundi madogo madogo. Pia Shuura inastawisha matumizi ya kanuni zinazotumika katika jumuiya nyingi; inahitaji mfumo au taratibu na sheria ambazo hazijaelewa katika sheria za Kiislamu. Muundo na namna ya kuendesha Shuura vimeachwa wazi, hata hivyo muundo wowote utakaotumika kuendeshea Shuura lazima uzingatie sheria za Kiislamu.

Kuna maoni tofauti juu ya misingi ya kitaasisi au ya kiulimwengu katika uanzishaji na matumizi ya Shuura katika mambo yanayohusu utawala na usimamizi kwa ujumla wake. Mambo hayo hayakufafanuliwa kwa kina katika sheria za Kiislamu. Hata hivyo zinaweza kupatikana kutoka katika sheria za Kiislamu na Shuura zilizofanywa wakati wa Mtume na kufuatwa na Makhalifa wake kwa mchakato wa kujifunza na utafiti.

Ufafanuzi ulio duni wa majukumu, mazingira na kazi za Shuura katika maisha ya Uislamu, yaliyoegemea katika tafsiri mahususi na matumizi ya maandiko ya kale, pia zilififisha idadi ya washiriki katika Shuura, ikielezwa kuwa Mtume alikaa Shuura yeye na maswahaba wengine wawili tu. Ukweli ni kwamba Mtume alikaa Shuura na idadi ya maswahaba ambayo haikutajwa, pia makundi mengine ya watu na hata mtu mmoja mmoja. Kuna mifano kadhaa ambayo Mtume anasema... “Enyi watu! Nishaurini”.

Aya mbili kutoka katika Qur’an zinazotengeneza msingi wa Shuura zinatoa mwongozo mzuri juu ya kuifahamu Shuura na mawanda ya matumizi yake miongoni mwa waumini wakiwemo wanawake. Misingi hii inatumika kwa wote labda ikiwa kuna ushahidi mahususi unaoonesha wanawake kutoshiriki. Katika sheria za Kiislamu amri na makatazo mengi yanawahusu wote wanaume na wanawake, hata ikiwa kiwakilishi cha nafsi kilichotumika kinaashiria mwanamme, umoja au wingi. Tunajua mazingira kadhaa ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu alikaa Shuura na maswahaba wa kike tu, hali kadhalika katika muktadha mwingine Mtume alikaa na maswahaba wake wa kiume na kike kwa pamoja, katika masuala muhimu sana yanayohusu vita, au maadili, au kuanzisha taratibu za Kiislamu.

Qur’an inatueleza mazingira mawili ambapo wanawake wamehusika katika Shuura. Mazingira yote mawili yanaonesha kutokatazwa na Mwenyezi Mungu; tukio la kwanza ni lile la Malikia wa Sheba akihitaji ushauri,⁹ na tukio la pili ni lile la mwanamke aliyemshawishi baba yake juu ya kumuajiri nabii Mussa – mtu mwaminifu.¹⁰ Wale wanaokataa mwanamke kushirikishwa katika masuala ya umma (kama vile bunge), wanasema wanawake hawaruhusiwi kukamata madaraka na kuwatawala wengine katika jamii. Mtazamo huu hauna mashiko,

9. Abu Bakar ibn al-‘Arabi, ‘Aridat al-Ahwadhi, fi Sharhi, Sahih al-Tirmidhi (Beirut: Dar al-Fikr li al-Tiba ‘ah wa al-Nashr wa al-Tawzi, hakuna tarehe), 7/206.

10. Qur’an 27:29-35.

uongozi wa mwanamke katika siasa na katika jeshi unaweza usiwe madhubuti ikiwa hatizamwi kuwa ni madhubuti na wale anaowaongoza, kwa sababu tu yeye ni mwanamke.

Shuura inaweza kuwa kwa watu mahususi katika nyakati fulani ama kwa kukusudia au bila kukusudia. Kuna watu wanaweza kuenguliwa katika Shuura kwa kuzingatia asili ya jambo lenyewe. Wanazuoni wanasema washauri hao ni wale wenye sifa ya uaminifu, taaluma na uzoefu juu ya jambo husika na (washauri hao) watachaguliwa kwa kura au kwa kupendekezwa. Njia ya kupendekeza ina faida kwa kuwa inatoa fursa kuchaguliwa mtu mahiri na mzoefu. Qur'an, Sunnah na wanazuoni wanaonesha kuwa mbinu zote zinaweza kutumika kwa pamoja, kipaumbele ikiwa ni kura. Ikiwa idadi ya washiriki ni ya kutosha na muafaka umefikiwa, basi hakuna haja ya kuendelea. Mwenyezi Mungu anamuamrisha Mtume

"fanya Shuura nao katika mambo yote ya kijamii, ikiwa muafaka juu ya jambo husika umepatikana, tawanyikeni mkimtegemea Mwenyezi Mungu.

(Al-Imran 3:159).

Shuura juu ya maswali na mambo mahususi iwahusishe watu wanaostahiki na walio na uwezo mkubwa wa kutoa mchango. Mambo haya mahususi ni yale yanayohusiana na sayansi, sheria, uchumi, mipango ya kijeshi na mengine mengi. Hivyo, unaweza kuona kuwa si kila mtu anaweza kushiriki katika mambo hayo.

Katika mazingira ya Kiislamu, Shuura (majilis al-Shuura) hufanywa na viongozi wa nchi na serikali. Katika baadhi ya nchi zetu za Kiislamu, Shuura hizo zimekuwa za kudumu sasa, hususani katika taasisi nyingi duniani. Shuura hizi huhusisha washauri wakuu ambao kwa kuzingatia kanuni za Shuura katika Uislamu lazima wawe na elimu, waaminifu na wazoefu.

Kumekuwa na mjadala na maswali mengi kuwa azimio linalotokana na Shuura linakuwa sheria au ni maoni tu. Ni kwa

namna gani yachukuliwe maoni ya watu wengi katika Shuura au maamuzi yanayoungwa mkono na watu wengi katika Shuura? Wanazuoni wa zamani waliona kuwa azimio litokanalo na Shuura kuwa ni maoni tu, kwa upande mwingine wanazuoni wa sasa wao wanaona kuwa kiongozi anapokaa Shuura na washauri wake basi inamuwajibikia kufungamana na azimio hilo.

Kuna dalili nyingi zitokanazo na Hadithi sahihi juu ya kushikamana na maoni yaliyoungwa mkono na wanashuura wengi. Pia, hili linaweza kuelezwa vyema katika Hadithi inayoeleza tukio la Mtume alipomwambia Abu Bakar na Omar, “Ikiwa nyinyi wawili mmekubaliana juu ya jambo fulani, basi mimi siwezi kwenda kinyume na ushauri wenu”.¹¹ Kwa mtazamo huo, azimio linalotokana na Shuura litastahiki kufuatwa na jamii yote.

Qur’an haijakataza juu ya kufungamana na maoni ya watu wengi yatokanayo na Shuura. Japo yapo mazingira fulani Qur’an imekataza kukubaliana na mawazo ya watu wengi, mawazo ya wazee au watu mashuhuri katika jamii ikiwaeleza kuwa ni watu wenye fikra potofu na waongo. Katika Hadithi za Mtume tunaonywa dhidi ya ubadhirifu unaofanywa na kundi la viongozi katika jamii za Waislamu hususani wasomi na viongozi wa kisiasa, ambao udhalimu wao unaweza kuiangamiza jamii kama ambavyo uadilifu wao unavyoweza kuiongoa jamii. Qur’an inasema kukubalika au kutokubalika kwa jambo hakutegemei uchache au wingi wa watu wanaounga mkono bali hutegemea uzuri na ubaya wa jambo lenyewe.

Malikia wa Sheba alisema asingeweza kufanya maamuzi mazito bila kuitisha Shuura ya washauri wake na tunaona kuwa hakuna mahala popote katika Qur’an jambo hilo lilipingwa. Sambamba na hilo kila tunachokiona katika maisha ya Mtume kinasadifu maneno ya Malikia. Malikia wa Sheba ameoneshwa

11. Qur’an 28:26.

katika Qur'an kama mfano mzuri wa mtawala ambaye maisha yake yaliishia katika kheri. Maneno na matendo ya Malikia yanadhihirisha ukweli kwamba alikuwa ni kiongozi mwema aliyetekeleza vyema majukumu aliyokasimiwa na Shuura, alikuwa mwanamke mwenye uzoefu, mwelewa na mwenye hekima.¹²

Kwa Mtume kutekeleza kanuni za Shuura katika maisha yake, inaunga mkono suala la kutekeleza fikra itokanayo na wanashuura walio wengi. Katika vita vya Badri, Mtume hakuwa tayari kuingia katika mapigano hadi alipoungwa mkono na Maswahaba walio wengi, muhajirina na wengineo. Katika vita vya Uhud, Maswahaba walio wengi walipinga mawazo ya Mtume hususan yale ya mkakati wa kimapambano. Mtume aliwasikiliza kisha akakubaliana na mawazo yao. Hivyo, huu ndio msingi wa mjadala juu ya azma itokanayo na Shuura kwamba je, mawazo ya wengi ni shuruti au kinyume chake?

Katika andiko moja, Mtume aliacha maoni yake na kukubaliana na maoni ya Maswahaba waliokuwa wengi. Jambo lile lilitokelezwa bila ya kupigiwa kura ya turufu, kubatilishwa wala kupingwa, baada ya tukio hili Mwenyezi Mungu alishusha aya akimuamrisha Mtume “fanya Shuura nao katika masuala yote yanayowahusu”. Andiko jengine linaonesha kwamba kushikamana na maoni ya walio wengi hata kama maoni hayo yanapingana na Imamu basi itakuwa si sahihi na ni kitendo kibaya kabisa.

Mtume mara zote alikuwa akitekeleza ibada hii ya Shuura, alikuwa akifanya majadiliano au kupokea mawazo ya watu kama inavyotarajiwa kwa mtu yeyote aliye Mtume wa Mwenyezi Mungu, anayepokea wahyi na maelekezo ya Allah. Katika matukio ambayo hayakuwa na maelekezo bainifu, Mtume hakusita kukaa Shuura.

12. Imesimuliwa na Imam Ahmad al-Musnad, 4/227. Tazama pia katika Ibn Hajar al-Asqalani, fath al-Bari, 15/284.

Suala la kuheshimu maoni ya walio wengi si jipya wala geni katika utamaduni wa Kiislamu na mfumo wa sheria ya dini ya Kiislamu. Kanuni ya kulipa uzito jambo lililokubalika na watu wengi limeungwa mkono na wanazuoni. Kwa mfano, wasomi wa Hadithi wanatilia mkazo juu ya kufungamana na maoni ya walio wengi. Pia, wanasheria wa Kiislamu wanakubaliana kuwa ikiwa wasomi hawakubaliani na jambo fulani, basi ni vyema kufungamana na mtazamo unaokubalika kwa walio wengi. Kanuni hiyohiyo ilitumika wakati wa Maswahaba.

Wale wenye elimu na uzoefu juu ya masuala fulani wawe mwongozo katika kufikia ukweli wa mambo hayo. Watoe mwongozo kwa kuzingatia misingi ya Qur'an na Hadithi na dhamira inayofungamana na mambo yenyewe. Uzuri na ukweli unaweza kufikiwa, ikiwa si mara zote basi kwa kiasi kikubwa ni kwa mtazamo huu wa kufungamana na azimio la walio wengi.

Ushahidi huo unatoka katika Qur'an, maisha ya Mtume Muhammad (s.a.w) na mifano kutoka kwa makhalifa waongofu, wasomi wa Hadithi, wanasheria na wanazuoni wa Kiislamu ambao muda wao mwingi wameutumia katika kusoma kanuni za falsafa za sheria za Kiislamu.

Sura ya Tatu



CHIMBUKO LA SHUURA NA HISTORIA YAKE

Sura hii inatazama uzoefu utokanao na historia ya Shuura katika jamii ya Kiislamu, kuona namna Shuura ilivyokuwa inatekelezwa wakati wa maisha ya Mtume na Makhalifa waongofu na katika karne zilizofuata, ambapo umma wa Kiislamu ulikuwa katika misukosuko. Misingi ya Shuura iliyowekwa katika vipindi vyote hivyo viwili vinatoa muongozo katika maisha yetu ya leo.

Mfumo wa Shuura ya Kiislamu katika nyakati zilizopita unatufunza mambo yafuatayo; Shuura inaonekana kama jambo la hiari, suala la mwitiko wa silka ya mtu mwenyewe, suala lililohalalishwa na sheria za Kiislamu na kurasimishwa katika matendo ya Kiislamu. Suala la Shuura katika kipindi cha mwanzo katika Uislamu lilisisitizwa na kutekelezwa kwa upana, lilifanywa juu ya mambo makubwa na madogo, kwa dhati na kwa uadilifu. Shuura kama ilivyofanywa na Mtume, ilifanywa pia na Maswahaba na Makhalifa waongofu.

Moja ya Shuura kubwa zilizowahi kufanyika baina ya mtu mmoja mmoja na vikundi vidogovidogo ni ile ya maandalizi ya uchaguzi wa mrithi wa kiti cha Mtume Muhammad (s.a.w) ambapo Abu Bakar aliteuliwa. Kuteuliwa kwa Abu Bakar, kiongozi shupavu, jasiri na mwenye imani thabiti kulifanywa kwa uwazi, bila malumbano wala mijadala kinzani. Abu Bakar alipozidiwa

na maradhi aliitisha Shuura ili kumpata mrithi wake pindi atakapofariki, hapa Omar aliteuliwa kumrithi. Baada ya Omar kudhuriwa, na hali yake kuwa mbaya zaidi, waumini walimshauri aitische Shuura ili wampate mrithi wake kama alivyofanya Abu Bakar. Omar aliridhia na kupendekeza watu sita ambao watakaa Shuura ili kumpata mrithi wake. Omar aliwateua watu hao kwa kuzingatia misingi ya sifa alizobainisha Mtume.¹¹

Jambo jengine linalohitaji Shuura ni mfano wa ugawanywaji wa majimbo yaliyotekwa toka kwa maadui wakati ule wa vita. Wanazuoni walizingatia masuala ya kisiasa, kijeshi na kiuchumi juu ya kuyagawa majimbo hayo, jambo ambalo lilileta mgongano baina ya Maswahaba. Omar (mpiganaji makini) na wengineo walijadiliana juu ya suala hili lakini haukupatikana muafaka. Hivyo, aliliweka jambo lile katika Shuura ya washauri wake. Aidha, aliungwa mkono dhidi ya fikra ya kuyagawanya majimbo iliyokuwa imependekezwa na wafuasi wake, wanazuoni na wasomi.

Katika zama hizi za mwanzo utekelezwaji wa Shuura ulifanywa kama suala la hiyari, uhuru wa kifikra, kujieleza na ubunifu katika kuhifadhi uhusiano uliopo katika jamii. Yapo matukio kadhaa katika zama za Maswahaba yanayotupa mifano hai; mfano, Omar na Abu Bakar walikataa kupitisha baadhi ya sheria bila kukaa Shuura na baadhi ya Viongozi wa Waislamu kujadili jambo hilo. Hili linaonesha ni kwa namna gani viongozi na watu wenye mamlaka wanapaswa kukaa Shuura juu ya mambo yenye munasaba na jamii.

Toka kipindi cha Makhalifa waongofu hadi kipindi cha utawala wa Umaiyya paligubikwa na mabadiliko ya kisiasa ndani ya jamii za Kiislamu. Japo Uislamu uliendelea kushinda katika nyanja mbalimbali kama vile; utamaduni, siasa, taaluma na jeshi, mabadiliko ya kisiasa kutoka katika utaratibu mzuri wa kuhitaji mashauriano uliowekwa na Makhalifa waongofu hadi utawala wa kimabavu unaotokana na kujirithisha madaraka, donda ambalo litachukua muda mrefu kutibika.

Moja ya maeneo ambayo ni muhanga wa mabadiliko yaliyozigubika jamii za Kiislamu kwa ujumla wake ni suala la Shuura lililoanzishwa katika misingi ya Qur'an, ilikuwa ndiyo mfumo wa maisha ya Mtume Muhammad (s.a.w) na makhalifa waongofu baada ya mtume.

Suala la Shuura bado halijawekewa misingi na utaratibu, japokuwa tunashuhudia maendeleo hasi na chanya ndani ya jamii za Waislamu na nchi za Kiislamu kwa ujumla. Mabadiliko haya yamelazimisha kutengenezwa kwa mipango mikakati, taasisi na mambo mengine katika mfumo mzima wa maisha ya Kiislamu. Mabadiliko yote hayo kama yanavyoonekana kukita katika mfumo, muundo na utaratibu mzima wa uongozi kulipelekea kupanuka kwa utawala wa Kiislamu kipindi cha Makhalifa waongofu. Maendeleo hayo, wakati mwingine yalitokana na utumiaji wa uzoefu kutoka tawala nyengine au ubunifu unaotokana na miongozo ya Qur'an na Sunnah. Kutokana na utaratibu huu, Uislamu ulipokea mifumo na miundo mipya au changamani katika nyanja zake za kisiasa, kiuchumi, kiutawala, kijeshi, kitaaluma, kisheria na mambo yake yote ya kijamii.

Nchi na jamii za Kiislamu zilitunga na kuboresha mifumo na mipango inayohitajika kufikia mahitaji yao ya kiimani na kimaumbile. Pamoja na yote hayo, suala la Shuura halikuwekewa mfumo na muundo wowote. Ilidhaniwa nguvu nyingi zingewekwa katika suala hili kutokana na umuhimu wake lakini haikuwa hivyo.

Hata mchakato wa kuchagua viongozi wa kisiasa na kidini katika jamii ya Waislamu umetolewa kabisa katika muundo wa Shuura kimatendo hata kinadharia. Isipokuwa maeneo machache, Shuura imekuwa haitekelezwi katika mambo muhimu na mipango ya kisiasa. Badala yake masuala yote ya kiutawala yameachwa katika mikono ya viongozi pekee ambao maslahi na utashi wao ndivyo vinavyoamua kila kitu. Na huu ndio umekuwa mfumo wa kisiasa ulioenea kote duniani.

Labda mfumo mzuri na utekelezwaji wa Shuura katika historia ya Uislamu unaonekana katika mfumo uliotawala wa mahakama za Kiislamu. Vinginevyo, mifumo ya mahakama iliyofuata inaonekana kwa maswahaba waongofu tu hususan kwa Omar na Othman. Mfumo huu wa Shuura mahakamani uliwekewa miundombinu mizuri hasa katika nchi za Andalusia na Morocco, ambapo Shuura ilikuwa sehemu muhimu ya mahakama. Katika mfumo huu, wanashuura wote waliteuliwa kama washauri, baada yakuwa wameteuliwa na hakimu au kiongozi anayetokana na wanasheria wa sheria za Kiislamu.

Ni eneo hili tu la mahakama ambapo Shuura imekuwa ikitekelezwa katika historia ya Uislamu. Mahakama imekuwa chombo pekee kilichoeleza mfumo wa maisha ya Kiislamu kwakuwa imeendelea kutumia hukumu zitokanazo na Qur'an na Sunnah. Historia inaonesha kuwa mataifa yaliyofanikiwa kisiasa bado yameshindwa kupiku muundo wa sheria za Kiislamu kimamlaka na kiutamaduni kutokana na mfumo wake huo thabiti.

Sura ya Nne



TUNAWEZAJE KUHAMASISHA UTEKELEZAJI WA SHUURA NA KUITUMIA KUJENGA USTAWI HIVI LEO?

Mambo mengi yanayohitaji Shuura si yenye kueleweka vizuri katika jamii na kanuni zake hazitekelezwi ipasavyo. Mabadiliko ya kimuundo yanayofanyika juu ya umuhimu wa Shuura utasaidia kuanzisha mfumo madhubuti wa Shuura. Hata hivyo, bado kunahitajika michango juu ya uanzishwaji wa mfumo wa Shuura na utekelezwaji wake katika nyanja mbalimbali.

Ili kuzifahamu vyema kanuni na mambo yanayoambatana na Shuura, namna nzuri itakayotuwezesha kupata amani katika maisha yetu hivi leo, lazima turejee nyuma na kuangalia misingi iliyowekwa na Mtume na Makhalifa wake waongofu.

Misingi hii ni pamoja na (1) nadharia na vitendo vinavyotokana na mifano iliyowekwa na Mtume, Maswahaba wake na Makhalifa wake waongofu, (2) kanuni na dhamira ya sheria za Kiislamu, (3) mambo yanayoambatana na mfumo wa Shuura na namna yalivyotekelezwa na Waislamu katika kipindi chote cha historia ulimwenguni kote.

Sehemu tunapopishana miongoni mwetu sisi Waislamu ni kwamba, uanzishwaji na utekelezaji wa Shuura unaambatana na dini ya Kiislamu na wahyi. Hivyo, ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ni moja ya misingi ya sheria. Hii inamaanisha kwamba

kuitekeleza Shuura ni sawa na kutekeleza sheria ya dini na kutoitekeleza vilevile ni kutotekeleza sheria ya dini. Waislamu wanaongozwa kwanza kwa misingi ya Qur'an na Sunnah na pili kupitia Shuura. Kunapotokea jambo linaloisibu jamii kwa ujumla au kuhusisha haki za baadhi ya wanajamii basi kuna haja kubwa ya kuwepo Shuura. Shuura hiyo ni lazima iwahusishe wale wanaoguswa na jambo lenyewe hasa inapoonekana kuwa hatima ya jambo hilo linaweza kuwaathiri.

Katika Uislamu hakuna nafasi ya mtu kuingilia kati mambo yaliyo katika miliki ya Mwenyezi Mungu, lakini hatuna hiari ya kushirikiana katika jumla ya mambo yanayotuhusu kama wanajamii, na hii ndiyo maana ya Shuura. Kupitia Shuura kila mmoja anapata nafasi ya kushiriki katika kufikiri, kuweka mipango na kusimamia mipango hiyo. Kila mmoja anapaswa kushiriki katika masuala haya na wale walio na mamlaka na madaraka wanawajibika kuwashirikisha wale wanaowatawala katika mchakato wa kufikiri, kuweka mipango na kusimamia mipango hiyo.

Ni haki ya kila Muislamu kushirikishwa katika masuala yanayomuhusu na yale aliyo na maslahi nayo. Hivyo, watu wana haki ya kushirikishwa katika Shuura, iwe moja kwa moja au kwa kuwakilishwa juu ya mambo yanayowahusu. Kwasababu hiyo, kuwanyima haki hii itakuwa ni udhalimu. Omar alikemea sana na hata kufikiria adhabu ya kifo juu ya kuwanyima raia haki ya kuwashirikisha katika mambo yanayowahusu.

Kwa kuzingatia hasara ambazo hazikuzungumzwa waziwazi, Waislamu wamekuwa wahanga kwa kushindwa kwao kutekeleza Shuura kama inavyotakiwa. Muda umefika sasa wa kuona umuhimu na thamani ya Shuura. Hata hivyo, lazima ifahamike kuwa Shuura ndiyo msingi wa pili baada ya Qur'an na Sunnah katika utekelezaji wa masuala yanayowahusu Waislamu. Hivyo, kuzungumzia udhalimu huu na kufufua mfumo madhubuti wa Shuura ni moja kati ya masharti ya kuihuisha imani na maumbile.

Shuura haijawahi kuwekewa mikakati madhubuti kama ilivyo vitengo mbalimbali katika mfumo wa serikali, uongozi, ugawaji wa zaka, hisbah¹³, mahakama, uzuiaji wa jinai, ulinzi na elimu¹⁴. Katika miaka ya mwanzo ya Uislamu uanzishwaji wa kipengele hiki cha Shuura ilikuwa si lazima wala muafaka kwa kuzingatia mazingira yenyewe. Hii ni kwakuwa Shuura ilifanywa kwa hiari tena kwa imani pasipokuwa na mfumo maalumu wa kudhibiti utekelezaji wa maamuzi, tena ilifanywa mara kwa mara na kwa umakini zaidi.

Shuura maana yake ni kuziweka sheria za Kiislamu, mantiki na ushirikiano katika maslahi ya pamoja miongoni mwa wanajamii. Shuura inahusisha, majadiliano, maelewano na makubaliano ambapo kila mmoja hupata fursa sawa. Pia, Shuura ni mchakato wa mabishano, kunasihiana na kumfanya kila mmoja kutumia ushahidi alionao juu ya kile anachokitetea. Hii inalazimisha uwepo wa sheria na taasisi ambayo itasimamia mfumo mzima wa Shuura. Ikiwa Uislamu haujaweka mfumo thabiti wa kusiamamia kitengo hiki cha Shuura basi kutatokea mabadiliko makubwa ambayo yatauharibu utaratibu mzima wa Shuura.

Katika aya nyingi za Qur'an na Hadithi tunaona kuwa suala la kutafuta elimu ni la lazima kwa kila Muislamu. Vilevile, tunaona kuwa Mtume (s.a.w) alituwekea mifano mizuri katika jamii ya Kiislamu juu ya Shuura na utafutaji wa elimu. Hivyo, tunapopambana katika kurejesha mfumo kamili wa Shuura kimatendo na kinadharia, hatuna budi kuchunga misingi na kanuni zilizojengwa juu yake.

Ushindi uliopatikana katika nyanja zote katika Uislamu na mataifa ya Kiislamu uligubikwa na machungu kadhaa kama vile ukosefu wa urari, okosefu wa hadhi na sifa za Uislamu, kupotea

13. Hisbah: Aina ya mamlaka ya kidini yanayoegemea katika kuamrisha kutenda mema na kukataza mabaya, iliyoibuka kama kazi huru enzi za Abbasid. Mtu aliyepewa majukumu haya alikuwa akisimamia masoko, usafi, na maadili katika jamii.

14. Adnan al-Nahwi, Malamih al-**Al-Shuura** fi al-Da'wah al-Islamiyyah (Damam: Dar al Islah li al- Tab' wa al- Nashr, hakuna tarehe) uk.36. Tazama pia katika Qur'an 27:43.

kwa uchamungu na kushuka viwango vya imani. Maswahaba na hata Waislamu waliofuata tabia kamili za Kiislamu hususan katika rasi ya Arabuni waliendelea kupungua siku hadi siku. Pia maeneo ya Levant, Iraq, Misri, Uajemi, Afrika Kaskazini na kwingineko, toka mauaji ya Omar na kama ilivyotokea kwa Othman na Ali. Nguvu ya Shuura iliyokuwa imefikiwa haikuwezesha kuweka mfumo madhubuti wa mwongozo wa Shuura.

Maendeleo yaliyofikiwa katika maisha ya watu na jamii kwa ujumla yanahitaji utumiaji wa fikra angavu. Lazima tuchukue hatua na kuanzisha taasisi zinazoweza kuichunga misingi ya dini ya Kiislamu na kuyalinda maslahi ya Waislamu dhidi ya vitisho na zahama zinazotishia maisha ya Waislamu.

Mafunzo tunayoyapata lazima yatokane na uzoefu wa kihistoria unaotokana na maadili na wema na changamoto zake, kwa ajili ya kuihuisha na kuipa nguvu Shuura. Uhuishaji huu unahitaji kuondoshwa kwa ombwe lililopo la utekelezwaji wa Shuura kama vile kuiwekea mfumo madhubuti wa kitaasisi.

Kuna kanuni nne za misingi ya sheria za Kiislamu ambazo pia zinaafikiana na maisha ya binadamu. Moja, inatokana na mfano kutoka kwa Omar alipogundua kuwa kulikuwa na mtu aliyekuwa tayari kutoa kiapo cha utii juu ya chaguo la mrithi wake baada ya kufa kwake. Baada ya kuona hatari ya dhamira hiyo, Omar alitangaza kuwa kiapo chochote cha utii kitakachotolewa bila ya Shuura baina ya Waislamu kitakuwa batili. Kwa ustadi na hekima, Omar alifunga kabisa mlango huu unaoweza kuibua mfarakano na migogoro. Alianzisha baraza la Shuura ambalo moja ya kazi zake ilikuwa ni kukusanya maoni ya umma kwa namna ambayo ilimpa fursa kila mmoja.

Kanuni ya pili ya *sadd al-dharā'i* ni kukataza kitu au mambo yoyote ambayo kimsingi yanaweza kupelekea kufanyika kwa uovu. Hii inakwenda mbali zaidi ya kanuni ya kwanza kwakuwa inapotokea aina yoyote ya makosa, hulazimika kupatikana kwa

hukumu. Kanuni hii ya pili ni mahsusi zaidi kwakuwa jambo halali linaweza kutumika katika mazingira ya kilichokatazwa. Kwa maneno mengine ni kwamba kitu kilicho halali na kinachoruhusiwa kinaweza kutumika katika mazingira zaidi ya yale yaliyokusudiwa. Kwa mfano, pamoja na ukweli kuwa Mtume aliwafahamu baadhi ya wanafiki na jitihada zao za kutaka kumdhuru Mtume na Waislamu, bado Mtume aliepuka kuwanyonga. Mtume aliwaacha kwa kuzingatia kanuni ya *ssadd al-dharā'i*.

Kanuni ya tatu katika mchakato wa utaratibu wa Shuura ni dhana ya maslahi ya umma (al-mursalāh) ambayo ni msingi kuntu katika sheria za Kiislamu. Dhana hii inahimiza dhana ya sheria ya Kiislamu kusimamia maslahi ya umma yawe ya kiimani au kimaumbile. Hukumu zote zinakusudia kuleta haki na kuwalinda watu dhidi ya madhara, iwe yanayojitokeza hapohapo au baadaye. Maslahi haya hayajaelezwa kwa undani katika Qur'an au katika Hadithi za Mtume bali huibuliwa na mazingira yanayoikabili jamii. Sheria kwa ujumla hazielezei kiundani maslahi yote ya binadamu wala kueleza fat-wa zote zinazotumika kulinda maslahi hayo ambazo kwa kiasi kikubwa zinaongezeka kila siku.

Kwa namna hiyo, sheria za kiislamu zimeainisha *fat-wa* na kanuni kwa ujumla zenye dhumuni la kusaidia kutatua changamoto za kimazingira zinazoibuka. Kila kitu ambacho ni kizuri, chenye faida na fadhila, sahihi na haki kinahitaji kuongozwa kwa misingi ya sheria ama kiwe kimehimizwa tu (*mandub*) au ni lazima kutekelezwa (*wajib*).

Hukumu za kiislamu lazima zitimize vigezo vifuatavyo; (1) lazima ziwiane na madhumuni ya sheria za kiislamu, zisikinane na maandiko matakatifu. (2) lazima zijitosheleze na zikidhi mantiki, ikiwa zinasomwa kwa watu wenye akili timamu basi zikubalike, na (3) ikiwa zitafanyiwa kazi basi zikidhi na kutimiza lengo la sheria. Kwa ujumla maslahi ya watu lazima yalindwe kwakuwa ndio msingi wa sheria za kiislamu. Misingi ya utungwaji wa

sheria za kiislamu imekuwa ikitekelezwa na wanasheria wa kiislamu, viongozi na mahakimu kusaidia jamii katika mazingira mbalimbali ya maisha. Mfano mzuri ni ukusanywaji wa Qur'an kipindi cha Khalifa Abu Bakar ikifuatiwa na kuiweka katika muundo wa kitabu ili kitumike kwa Waislamu wote katika nchi zao kipindi cha utawala wa khalifa Othman ibn Affan.

Kanuni ya nne ya muundo wa Shuura ni ukopaji kutoka katika miundo mingine kwa dhamira njema. Kanuni hii hukidhi viwango vya sheria za kiislamu na imekuwa ikitumika kipindi chote katika historia ya Uislamu. Ilitumika pia wakati wa Mtume, Maswahaba wake, Makhalisa waongofu na Waislamu wote kwa ujumla katika zama zote hususani juu ya masuala ya kiutawala. Waislamu walizichukua kanuni hizo toka katika mifumo mingine pale tu zilipothibitika kutokinzana na dini ya Kiislamu. Vigezo vilivyotumika kuzipima ili zipate kuigwa zilizingatia iwapo kanuni hizo zilifaidisha na kuyalinda maslahi ya umma.

Kwa kuzingatia Shuura kama zana ya kuleta mabadiliko, mjadala huu unaakisi kabisa mwamko na mwitikio wa kisiasa na kijamii, wakati huohuo ikidumisha lengo lake. Ni kwa namna gani sasa kanuni hizi za mabadiliko zitiwe katika vitendo ili zichochee maendeleo? Hapa hatuna budi kujijengea utamaduni wa kukaa Shuura.

Uhimizaji wa utamaduni wa kukaa Shuura unahitaji uandikaji wa vitabu na makala nyingi, mihadhara mingi, semina na makongamano mengi yenye lengo la kuamsha hisia za Waislamu juu ya umuhimu wa Shuura na changamoto zake ili kutekeleza ibada hii ya Shuura. Suala hili litafanikiwa kwa kutumia miundombinu yoyote inayowezekana kama vile vyombo vya habari, kuelimishana, kupeana maelekezo, mihadhara na fatwa na kadhalika. Ikiwa makundi ya jamii na taasisi zitatekeleza mpango huu hakika zitachochea utamaduni wa ukaaji wa Shuura baina ya Waislamu.

Hitimisho



Kiwa mtu mmoja mmoja au katika makundi watatekeleza ibada hii ya Shuura, bila shaka watakuwa wamejenga misingi na nguzo imara ya kanuni za Kiislamu. Hebu tushikamane na aya ya Qur'an (42:38) inayosema ¹⁵ na Waislamu ambao katika mambo yao yote huyafanya kwa Shuura baina yao¹⁶ iliyoshuka kwa kundi dogo la waumini ambao walikuwa wakiwaita watu katika imani ya Kiislamu na ambao hawakuwa na nchi.

Mwitiko huu unahitaji kujenga misingi ya Shuura kuwa tabia endelevu ya maisha yetu kwa ujumla. Tabia ya kutekeleza ibada hii ya Shuura itadumu ikiwa tutaishi katika mazingira ya amani, kujitambua, uhuru wa kimawazo na uhuru wa kuzungumza.

15. Adnan al-Nahwi, Malamih al-**Al-Shuura** fi al-Da'wah al-Islamiyyah (Dam-mam:Dar al Islah li al- Tab' wa al- Nashr, hakuna tarehe) uk.36.Tazama pia katika Qur'an 27:43.

16. Sahihi al-Bukhari, Kitabu cha Maadili (kitab al-fada'il), mlango haukutajwa, "Kisa cha kuanza kwa utii kwa Othmani na makubaliano ya uteuzi wake".

Maelezo Ya Pembeni



- 1 Imesimuliwa na al-Tirmidhī katika moja ya milango yake ya jihadi.
- 2 Ingawa kulikuwa na udhaifu katika mlolongo wa masimulizi haya maudhui yake yamethibitishwa kuwa ya kweli na yakuaminika, pia, ‘Abu ‘Umar ibn ‘Abd al-Barr, Jamii’ Bayan al-Ilm wa Fadlihi wa Yanbaghi fi Riwayatihī wa Hamlihi (Beirut: Dar al – Fikr, hakuna tarehe), 2/73.
- 3 Sahih al Bukhari, Kitabu cha wito wa Sala (kitab al-adhan), na al-Tirmidhi, Mlango wa Sala (abwab al-Sala).
- 4 Muhammad Ruwwas Qalaji, Mawsu ‘at Fiqhi Abi Bakar al-Siddiq (Beirut: Dar al Nafa ‘is, 1994), uk. 155.
- 5 Abu Bakar al Jassas, Ahkam al Qur’an, 2/41.
- 6 Abu Bakar ibn al-‘Arabi, ‘Aridat al-Ahwadhi, fi Sharhi, Sahih al-Tirmidhi (Beirut: Dar al-Fikr li al-Tiba ‘ah wa al-Nashr wa al-Tawzi, hakuna tarehe), 7/206.
- 7 Qur’an 27:29-35.
- 8 Qur’an 28:26.
- 9 Imesimuliwa na Imam Ahmad al-Musnad, 4/227. Tazama pia katika Ibn Hajar al-Asqalani, fath al-Bari, 15/284.
- 10 Adnan al-Nahwi, Malamih al-Shura fi al-Da’wah al-Islamiyyah (Dammam: Dar al Islah li al- Tab’ wa al- Nashr, hakuna tarehe) uk.36. Tazama pia katika Qur’an 27:43.
- 11 Sahih al-Bukhari, Kitabu cha Maadili (kitab al-fada’il), mlango haukutajwa, “Kisa cha kuanza kwa utii kwa Othmani na makubaliano ya uteuzi wake”.
- 12 Hisbah: Aina ya mamlaka ya kidini yanayoegemea akika kuamrisha kutenda mema na kukataza mabaya, iliyoibuka kama kazi huru enzi za Abbasid. Mtu aliyepewa majukumu haya alikuwa akisimamia masoko, usafi, na maadili katika jamii.
- 13 Qur’an 42:38.

KUHUSU MWANDISHI

AHMAD AL-RAYSUNI ana digrii ya Uzamivu katika Taaluma za Dini ya Kiislamu kutoka katika Chuo Kikuu cha Muhammad al-Khamis, Rabat, nchini Morocco. Amefanya kazi katika Wizara ya Sheria, ni mhariri wa gazeti la al-Tajdid, na ni mwanachama Jumuiya ya Wanazuoni wa Kiislamu nchini Morocco.

Profesa al-Raysuni ameandika vitabu vingi na makala nyingi katika *al-Maqaid* kwa Kiarabu, ambazo miongozi mwazo zimetafasiriwa katika lugha nyingine. Kwa sasa Profesa Raysuni anafundisha Usul al-Fiqh na Maqasid al-Shari'ah katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii katika Chuo Kikuu cha Muhammad al-Khamis, Morocco.

Waislamu, kwa kiwango kikubwa hawakutambuwa umuhimu na thamani ya kanuni ya *Shuura* iliyomo kwenye Qur'an, pamoja na kazi kubwa inayoweza kufanya katika kuiendeleza na kuijenga upya jamii ya Kiislamu.

Katika kitabu hiki, mwandishi amethubutu kubainisha maana halisi ya *Shuura* na kuchambua vipengele vya utekelezaji wake. Amedhihirisha chimbuko la *Shuura* na kuonesha namna ambavyo kanuni hii inavyoweza kuingizwa, kutekelezwa katika taasisi na jumuiya, na kutumiwa na jamii za Waislamu kwa ujumla.

Mambo haya na mengine mengi yamefanyiwa utafiti makini wa kitaalamu unao dhihirisha kwamba, Waislamu lazima wafanye *Shuura* kuwa mfumo wao wa maisha ili kulinda maslahi yao, na kwamba *Shuura* ni zana muhimu kwa wao kuweza kujijenga na kujiimarisha upya.

AHMAD AL-RAYSUNI 2012 AD



IITI — Mfululizo wa Vitabu kwa Muhtasari